# SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

## MUHTASARI WA

# HISTORIA

## KWA SKULI ZA MSINGI

## DARASA LA V – VI

**2009**

**© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, 2009**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigisha chapa au kutoa muhtasari huu kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

**Umetayarishwa na:**

**IDARA YA MITAALA NA MITIHANI**

**S.L.P. 3070**

**ZANZIBAR**

## YALIYOMO

Ukurasa

**UTANGULIZI** ........ iii
Sababu za Kuandika Mtaala Mpya wa Elimu ya Msingi ........ iv
Umuhimu wa Somo la Historia ........ v
Madhumuni ya Elimu Zanzibar ........ v
Madhumuni na Malengo ya Elimu ya Msingi ........ vi
Ujuzi wa Jumla wa Somo la Historia ........ vii
Malengo ya Jumla ya Somo la Historia ........ vii
Uchaguzi na Mpangilio wa Mada ........ viii
Muundo wa Muhtasari ........ ix
**DARASA LA TANO** ........ 1
UJUZI ........ 1
MALENGO ........ 1
**DARASA LA SITA** ........ 29
UJUZI ........ 29
MALENGO ........ 30

## UTANGULIZI

Muhtasari huu ni wa somo la Historia ambalo katika mtaala mpya (2009) litafundishwa katika Darasa la V na VI. Katika mtaala wa 1998 ambao umedumu hadi 2009, mada za somo la Historia zilikuwa zikifundishwa kwa madarasa ya IV hadi VII katika somo la Sayansi Jamii. Katika utangulizi huu unatolewa ufafanuzi wa sababu za kuandika mtaala mpya wa elimu ya msingi. Kisha kuna orodha za Madhumuni ya Elimu Zanzibar na Malengo ya Elimu ya Msingi; ujuzi unaotarajiwa kuoneshwa na walengwa na malengo ya kufundisha somo hili. Mwisho kuna maelezo ya uchaguzi na mpangilio wa mada pamoja na ufafanuzi wa muundo wa muhtasri na vipengele vyake.

### Sababu za Kuandika Mtaala Mpya wa Elimu ya Msingi

Mnamo mwaka 2008/2009 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliendesha mchakato wa kufanya mapitio, kufupisha na kuandika upya mtaala wa elimu ya msingi. Madhumuni yalikuwa ni kufanya mtaala ushabihiane na Sera ya Elimu ya Zanzibar (2006). Sera inalenga, kwanza, kurekebisha ubora na muundo wa elimu ya msingi. Pili, inalenga kuweka muunganiko bayana kati ya elimu ya msingi, maandalizi na sekondari ili kukidhi matarajio ya walengwa na jamii yao. Kwa hiyo, Sera ya Elimu ya 2006 imebadili muundo wa elimu kwa kuifanya elimu ya maandalizi kuwa ni sehemu ya elimu ya lazima. Vile vile imepunguza muda wa elimu ya msingi kutoka miaka saba (7) na kuwa miaka sita (6). Aidha, baadhi ya masomo katika elimu ya msingi yatafundishwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza kwa madarasa ya V na VI.

Mambo mengine yaliyochochea mapitio haya ni pamoja na yafuatayo:

- Mwelekeo wa kilimwengu katika maendeleo ya kijamii, kisayansi na kiteknolojia.
- Mwitiko wa serikali kwa Wazanzibari kudai nafasi zaidi za skuli kwa watoto wote na kuongeza ubora wa elimu inayotolewa.
- Mwitiko wa serikali kwa matokeo ya *Utafiti wa Mahitaji katika Mtaala wa Elimu ya Msingi* wa 2008.

Utafiti wa 2008 ulizingatia mapungufu yafuatayo katika mtaala wa 1998:

- Mtaala wa 1998 haukukuza stadi za kuwasiliana, ubunifu na fikra yakinifu.
- Haukuzingatia vya kutosha mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu na masuala mtambuka.
- Ulihimiza matumizi ya mbinu za kufundishia/kujifunzia zilizojikita kwa mwalimu zaidi kuliko kwa mwanafunzi.

- Ufundishaji/ujifunzaji ulikuwa wa kinadharia zaidi kuliko kuwa wa vitendo au ushiriki wa wanafunzi.

Kutokana na changamoto kama hizo serikali ilifanya maamuzi kadhaa kuhusu mustakabali wa mtaala wa Elimu ya Msingi. Mojawapo ni kuwapatia wanafunzi mtaala unaohimiza utendaji au unaokuza stadi anuai. Iliamuliwa pia kurejesha masomo ya Historia, Jiografia na Uraia katika mtaala. Vile vile yalitolewa maelekezo ya kuhakikisha kwamba mada za masomo ya Elimu ya Msingi zinaungana bayana na za elimu ya maandalizi na ya sekondari.

**Umuhimu wa Somo la Historia**

Somo la Historia linafundishwa kwa sababu kuu zifuatazo. Kwanza, ni kuwezesha walengwa kuelewa chimbuko la jamii yao na jamii nyengine. Pili, ni kuelewesha mambo yaliyosababisha mabadiliko ya kihistoria Zanzibar, Tanzania, barani Afrika na kwengineko Ulimwenguni. Maarifa haya ya mambo yaliyopita huwasaidia kuelewa mambo ya wakati uliopo na ujao. Tatu, ni kuwezesha wanafunzi kuchambua na kuthamini utamaduni wao na kuudumisha. Nne, ni kukuza uzalendo au upendo kwa taifa lao na kudumisha umoja. Tano, ni kuwapatia wanafunzi stadi za kihistoria ili waweze kujitegemea kifikra na kimatendo.

**Madhumuni ya Elimu Zanzibar**

Yafuatayo ndiyo madhumuni ya elimu:

1. Kukuza na kudumisha tabia na desturi bora za Wazanzibari na Watanzania ili kuimarisha umoja na utambulisho wao wa kiutamaduni.
2. Kuimarisha upatikanaji na matumizi sahihi ya aina mbalimbali za maarifa, stadi na mwelekeo/mwenendo kwa ajili ya kuendeleza kikamilifu utu na ubora wa maisha ya jamii.
3. Kuwezesha kila mwananchi kuelewa na kuheshimu misingi ya Katiba ya Zanzibar na ya Tanzania, Haki za Binadamu, pamoja na haki, wajibu na majukumu ya kiraia.
4. Kuendeleza na kuhimiza matumizi bora, uangalizi na utunzaji wa mazingira.

5. Kukuza utashi na heshima ya kufanya kazi za kujiajiri na kuajiriwa pamoja na nidhamu kazini na utendaji kazi kwa kiwango cha juu cha ubora.
6. Kukuza na kudumisha misingi ya kuvumiliana, amani, upendo, haki, maelewano, haki za binadamu na uhuru, umoja wa kitaifa na kimataifa kama vinavyofafanuliwa katika mikataba ya kimataifa.

**Madhumuni na Malengo ya Elimu ya Msingi**

Yafuatayo ndiyo madhumuni na malengo ya Elimu ya Msingi Zanzibar:

1. Kuwezesha watoto wote wenye umri wa kwenda skuli kujenga na kudumisha misingi imara ya stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu, ubunifu na mawasiliano kwa lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha nyengine za kigeni.
2. Kuwezesha wanafunzi kuelewa matumizi ya sayansi na teknolojia na kutambua mchango wake katika maendeleo ya taifa lao na ulimwengu.
3. Kuweka, kuendeleza na kudumisha miongoni mwa wanafunzi misingi imara ya stadi za kufikiri na udadisi ili kuelewa mazingira yao na uhusiano ya kijamii.
4. Kuwezesha wanafunzi kuelewa jinsi matukio yaliyopita yanavyoathiri matukio ya wakati uliopo na ya wakati ujao.
5. Kugundua vipaji vya kila mwanafunzi kuanzia umri mdogo ili kuvidumisha na kuviendeleza.
6. Kuweka misingi imara ya stadi za uchunguzi, fikra na ushirikiano katika kutatua matatizo yanayodumaza maendeleo binafsi ya wanafunzi na ya jamii yao.
7. Kuwaandaa wanafunzi kujiunga na elimu ya sekondari.
8. Kuwezesha wanafunzi kukuza uwezo wao kiakili na utashi wa kujitafutia maarifa.
9. Kuwazoesha wanafunzi shughuli za uzalishaji mali na kukuza ari yao katika kutekeleza majukumu ya kijamii.
10. Kuwezesha wanafunzi kutambua na kuenzi umoja wa taifa lao pamoja na ushirikiano baina ya taifa lao na watu na mataifa mengine.
11. Kuwezesha wanafunzi kujenga maadili mema kiroho, kiutamaduni na kiitikadi ili kukuza uzalendo na ufahamu wa hali ya nchi yao kihistoria, kisiasa na kijamii.

12. Kukuza na kudumisha nidhamu binafsi ya wanafunzi, kuheshimu usawa wa kijinsia na kulinda afya zao na za watu wengine.
13. Kuwezesha wanafunzi kujenga tabia za umaridadi na unadhifu pamoja na matumizi bora ya muda wao wa mapumziko.
14. Kukuza upendo wa wanafunzi kwa mazingira wanamoishi pamoja na utashi wa kuyatunza.

**Ujuzi wa Jumla katika Somo la Historia**

Mtaala huu umejikita katika kumpatia ujuzi mwanafunzi (badala ya kujikita katika kufundisha maudhui tu). Ujuzi ni muunganiko sawia wa maarifa, stadi na mwenendo/mwelekeo anavyotarajiwa kuvipata mwanafunzi. Kwa hiyo, baada ya kusoma somo la Historia hadi Darasa la VI wanafunzi wataonesha ujuzi wa:

1. Kubainisha na kueleza hatua za maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya binadamu katika nyakati mbali mbali.
2. Kubainisha na kueleza taarifa za uhusiano kati ya Wazanzibari na jamii za nje na athari zake hadi 1880.
3. Kukusanya na kueleza taarifa za uhusiano kati ya Watanganyika na jamii za nje na athari zake hadi 1880.
4. Kubainisha na kueleza shughuli za vitangulizi vya wakoloni katika Zanzibar na Tanganyika na athari zake.
5. Kukusanya na kueleza taarifa za athari za ukoloni katika historia ya Zanzibar, Tanganyika na Afrika kwa ujumla.
6. Kubainisha na kueleza sababu, juhudi na harakati za ukombozi Zanzibar.
7. Kubainisha na kueleza sababu, juhudi na harakati za kupigania uhuru Tanganyika na kwingineko Afrika.
8. Kubainisha na kueleza mafanikio na matatizo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi baada ya Mapinduzi ya Zanzibar.
9. Kubainisha na kueleza mafanikio na matatizo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi baada ya uhuru Tanganyika na kwingineko Afrika.
10. Kutumia maktaba na vifaa vya TEHAMA (teknolojia ya habari na mawasiliano)ili kutafuta maarifa na stadi za kihistoria.

**Malengo ya Jumla ya Somo la Historia**

Somo la Historia linafundishwa katika skuli za msingi ili kuwezesha wanafunzi:

1. Kufahamu maendeleo ya kijamii na kiteknolojia katika Zama za chuma.
2. Kuelewa uchambuzi wa uhusiano kati ya Wazanzibari na jamii za nje na athari zake hadi 1880.
3. Kuelewa uhusiano kati ya Watanganyika na jamii za nje na athari zake hadi 1880.

4. Kufahamu madhumuni ya ujio wa vitangulizi vya ukoloni na athari zake.
5. Kufahamu madhumuni ya uvamizi na ukoloni katika Zanzibar, Tanganyika na kwingineko Afrika na maelezo ya athari zake.
6. Kufahamu uchambuzi wa juhudi za harakati za ukombozi wa Zanzibar.
7. Kufahamu uchambuzi wa juhudi za kudai uhuru Tanganyika na kwingineko Afrika na maelezo ya sababu zake.
8. Kujua tathmini ya mafanikio na matatizo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa Afrika baada ya uhuru.
9. Kupata maarifa na stadi za kihistoria kupitia katika matumizi ya maktaba na vifaa vya TEHAMA.

**Uchaguzi na Mpangilio wa Mada**

Mada zilizochaguliwa zinalenga kumpatia mwanafunzi maarifa, stadi na mwelekeo uliokusudiwa katika ujuzi wa jumla wa somo na wa kila darasa. Mada kuu na mada ndogo zimepangwa kimantiki kuzingatia umuhimu wa maudhui na mfuatano wake kihistoria. Aidha umezingatiwa uwezo wa wanafunzi kiakili na ukaribu wa kila tukio la kihistoria kwa mazingira na maisha ya mwanafunzi. Ufuatao ndio mpangilio wa mada za Historia kati ya Darasa la V na la VI.

| **MADA KUU ZA DARASA LA V** | **MADA KUU ZA DARASA LA VI** |
|---|---|
| 1. Zama za chuma. | 1. Ukoloni katika Nchi Nyingine za Afrika. |
| 2. Mifumo ya Kiuchumi na Kiutawala katika Zanzibar na katika Tanganyika hadi 1880. | 2.Harakati za Kudai Uhuru wa Zanzibar. |
| 3. Uingiaji wa Wageni Zanzibar. | 3. Harakati za Ukombozi Zanzibar. |
| 4. Uingiaji wa Wageni Tanganyika na Athari zake. | 4.Harakati za Kudai Uhuru wa Tanganyika. |
| 5. Vitangulizi vya Ukoloni. | 5.Muungano wa Zanzibar na Tanganyika. |
| 6. Kugombaniwa na Kugawanywa kwa Afrika. | 6.Ukombozi wa Nchi Nyingine za Afrika – Ghana, Zimbabwe na Msumbiji. |
| 7. Uvamizi wa Kikoloni Zanzibar na Tanganyika. | 7. Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru. |
| 8. Ukoloni Zanzibar na Tanganyika. | |

**Muundo wa Muhtasari**

Muhtasari huu una sehemu kuu mbili: Kurasa za Mwanzo na jadweli za Ufundishaji na Ujifunzaji.

**Kurasa za mwanzo**

Sehemu hii inajumuisha jalada, ukurasa wa jina la muhtasari, ukurasa wa haki-miliki na wa yaliyomo. Vile vile, kuna sababu za kuandika mtaala mpya wa elimu ya msingi na maelezo ya umuhimu wa somo la Historia. Kisha kuna orodha za madhumuni ya Elimu Zanzibar; Madhumuni ya Elimu ya Msingi Zanzibar, ujuzi katika somo la Historia na malengo ya somo la Historia. Mwisho kuna maelezo kuhusu uchaguzi na mpangilio wa mada na ya muundo wa muhtasari.

**Jadweli ya Ufundishaji na Ujifunzaji**

Sehemu hii inaonesha utaratibu wa ufundishaji na ujifunzaji na imegawika katika madarasa mawili. Muhtasari wa kila darasa umetanguliwa na ujuzi ambao wanafunzi wanatakiwa kuonesha katika darasa husika. Kisha kuna malengo yanayotazamiwa kufikiwa katika darasa hilo. Baada ya malengo linafuata jadweli la ufundishaji/ujifunzaji lenye safu - wima sita zenye vichwa vya: Mada Kuu/Mada Ndogo; Malengo Mahsusi; Mbinu za Kufundishia/Kujifunzia; Vifaa/Zana; Upimaji na Vipindi kwa kila mada ndogo.

Inashauriwa kwamba katika kupanga utaratibu wa ufundishaji/mfululizo wa mada na mada ndogo uliopo katika muhtasari ufuatwe. Yafuatayo ni maelezo ya maudhui ya safu – wima za jadweli za ufundishaji/ujifunzaji.

***Mada Kuu/Mada Ndogo***

Mada hutamka maudhui yatakayofundishwa. Chini ya mada kuna mada ndogo ambazo huonesha kina na mawanda ya ufundishaji/ujifunzaji wa mada husika.

***Malengo Mahsusi***

Kila mada ndogo imeandikiwa lengo mahsusi au malengo mahsusi. Malengo haya yanazingatia ujenzi wa ujuzi uliokusudiwa pamoja na kufikia malengo makuu ya somo. Kila lengo mahsusi linatamka mambo ambayo mwanafunzi anatarajiwa aweze kufanya baada ya kujifunza/kufundishwa mada husika. Kila mwanafunzi darasani anatakiwa kuyafikia malengo mahsusi yaliyotajwa. Hivyo mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa lugha ya alama inatumiwa kumfundisha mwanafunzi kiziwi na mashine ya Braille au zana mguso zinatumiwa kwa mwanafunzi asiyeona. Kwa ufundishaji/ujifunzaji wa makundi mengine ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu mwalimu atumie taratibu na miongozo iliyopo, vifaa na mbinu zinazostahiki.

***Mbinu za Kufundishia/Kujifunzia***

Safu hii inaonesha baadhi ya mbinu zinazofaa kufundishia/kujifunzia. Ni mbinu shirikishi tu zinazopendekezwa. Hii ni kwa sababu zinahimiza wanafunzi kujitafutia maarifa na kujenga maana kwa kile wanachojifunza. Mbinu hizo ni kama vile majadiliano ya vikundi; maigizo; nyimbo; changanyakete; bungua-bongo; ziara za kielimu, kumwalika mgeni na nyingine ambazo mwalimu anaweza kuzitumia kutegemea mazingira, mada na umri wa wanafunzi. Mbinu zilizomo katika safu hii ni mapendekezo tu. Mwalimu anashauriwa atumie mbinu nyengine anazozimudu zitakazoshirikisha wanafunzi na kufanikisha ufundishaji/ujifunzaji.

***Vifaa/Zana***

Safu hii imesheheni mapendekezo ya zana na vifaa ambavyo vinafaa kutumiwa katika kufundisha/kujifunza kila mada. Kitabu cha kiada na kiongozi cha mwalimu ni zana muhimu pia. Mwalimu anashauriwa kuzitumia hizi pamoja na nyegine atakazoona zinafaa au zinapatikana katika mazingira yake. Aidha, mwalimu anashauriwa kubuni na kutengeneza zana/vifaa kulingana na upatikanaji wa malighafi katika mazingira yake. Pia anashauriwa kuwaongoza wanafunzi kutengeneza zana zao za kufundishia/kujifunzia.

***Upimaji***

Safu hii inaonesha maelekezo ya upimaji wa wanafunzi. Inampasa mwalimu kupima maendeleo ya kila siku ya wanafunzi wake. Hii itamwezesha kujua uwezo na matatizo ya wanafunzi, ubora wa mbinu za kufundishia/kujifunzia anazozitumia na ubora wa zana/vifaa anavyotumia. Vile vile upimaji humwezesha mwalimu kupanga na kutekeleza mikakati ya kuwasaidia wanafunzi wazito. Aidha upimaji humwezesha mwalimu kupendekeza marekebisho ya mtaala na vitabu vya kufundishia/kujifunzia. Upimaji wa mwisho wa muhula au mwaka huonesha kiwango cha ujuzi alichofikia mwanafunzi.

Kwa sababu hizo, mwalimu anashauriwa kupima maendeleo ya mwanafunzi kila siku, kila mwezi, kila muhula na kila mwaka kwa kuzingatia malengo mahsusi ya kila mada iliyofundishwa na njia mwafaka za upimaji.

***Vipindi***

Safu - wima hii inaonesha idadi ya vipindi vilivyokadiriwa kufundisha kila mada ndogo. Makadirio hayo yamefikiwa baada ya kujumlisha idadi ya vipindi kwa mwaka wa masomo na kuvigawa na idadi ya mada ndogo zilizomo katika muhtasari. Tofauti ya idadi ya vipindi imezingatia kina cha mada ndogo na idadi ya malengo mahsusi yanayoihusu. Hata hivyo, mwalimu anaweza kurekebisha mgawanyo wa idadi ya vipindi kwa mada ndogo kwa kutegemea mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wake. Vipindi vinne (4) vimepunguzwa kwa ajili ya majaribio na mitihani.

Somo la Historia lina vipindi viwili (2) kwa wiki. Muda wa kipindi kimoja kuanzia Jumatatu hadi Alhamisi ni dakika 40 kwa shifti ya asubuhi; ni dakika 35 kwa shifti ya mchana. Siku ya Ijumaa muda wa kila kipindi utakuwa dakika 30 tu. Utawala wa skuli unatakiwa kufidia muda wa masomo utakaopotea kutokana na dharura, sikukuu za kidini au sikukuu za kiserikali.

**KATIBU MKUU**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

**ZANZIBAR**

## DARASA LA TANO

### UJUZI

Baada ya kusoma somo la Historia katika Darasa la V wanafunzi wataonesha ujuzi wa:

1. Kubainisha na kuelezea maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Zanzibar na Tanganyika katika Zama za chuma.
2. Kubainisha na kueleza taarifa kuhusu uhusiano kati ya Wazanzibari na jamii za nje kabla ya 1880.
3. Kubainisha na kueleza taarifa kuhusu uhusiano kati ya Watanganyika na jamii za nje kabla ya 1880.
4. Kuainisha na kueleza malengo na athari za ujio wa vitangulizi vya ukoloni Tanzania na kwingineko Afrika.
5. Kutumia matumizi ya maktaba na vifaa vya TEHAMA ili kupata maarifa na stadi za kihistoria.

### MALENGO

Malengo ya kufundisha somo la Historia katika Darasa la V ni kuwezesha wanafunzi:

1. Kufahamu maendeleo ya binadamu kiuchumi na kijamii katika Zama za chuma.
2. Kuelewa uhusiano kati ya Wazanzibari na jamii za Asia na Ulaya na athari zake hadi 1880.
3. Kuelewa uhusiano kati ya Watanganyika na jamii za Asia na Ulaya na athari zake hadi 1880.
4. Kufahamu madhumuni ya vitangulizi vya ukoloni Afrika na athari zake.
5. Kufahamu matumizi ya maktaba na vifaa vya TEHAMA ili kupata maarifa na stadi za kihistoria.

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. ZAMA ZA CHUMA<br>a) Ugunduzi wa Chuma. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza maana ya zama za chuma. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya zama za chuma. | 1. Picha za zana za chuma. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maana ya zama za chuma? | 2 |
| | (ii) Kuzitaja sehemu za mwanzo zilizopata utaalamu wa chuma katika Afrika Mashariki. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kujisomea katika maktaba mwalimu awaongoze wanafunzi kupata maarifa kuhusu sehemu za mwanzo zilizopata utaalamu wa chuma katika Afrika Mashariki.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja sehemu za mwanzo zilizopata utaalamu wa chuma katika Afrika Mashariki. | 1. Vitabu vya kiada.<br>2. Makala yenye taarifa za zama za chuma.<br>3. Makala katika maandishi ya Braille.<br>4. Ramani ya Afrika Mashariki.<br>5. Ramani mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kuzitaja sehemu za mwanzo zilizopata utaalamu wa chuma katika Afrika Mashariki? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| b) Kuenea kwa Utaalamu wa Chuma. | Mwnafunzi aweze:<br>(i) Kueleza namna utaalamu wa chuma ulivyoenea. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kujisomea katika maktaba kwa vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kukusanya taarifa za namna ya utaalamu wa chuma ulivyoenea.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza namna utaalamu wa chuma ulivyoenea. | 1. Vitabu vyenye taarifa za zama za chuma.<br>2. Vitabu katika maandishi ya Braille.<br>3. Ramani ya Afrika Mashariki.<br>4. Ramani mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza namna ya utaalamu wa chuma ulivyoenea? | 3 |
| | (ii) Kueleza matokeo ya kuenea kwa utaalamu wa chuma. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kupata maarifa kuhusu matokeo ya kuenea kwa utaalamu wa chuma.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi waweze kueleza matokeo ya kuenea kwa | 1. Kitini chenye taarifa za zama za chuma.<br>2. Kitini katika maandishi ya Braille.<br>3. Picha mbali mbali za zana za chuma.<br>4. Picha za shughuli mbali mbali za | Je, mwanafunzi anaweza kueleza matokeo ya kuenea kwa utaalamu wa chuma? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | utaalamu wa chuma. | kiuchumi.<br>5. Picha mguso za zana na shughuli za kiuchumi. | | |
| c) Umuhimu wa Matumizi ya Chuma. | Mwanafunzi aweze kueleza umuhimu wa matumizi ya chuma. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza umuhimu wa matumizi ya chuma. | 1. Picha za zana za kilimo.<br>2. Picha za silaha za chuma.<br>3. Picha mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza umuhimu wa matumizi ya chuma? | 3 |
| d) Mabadiliko ya Kimaendeleo katika Zama za Chuma. | Mwanafunzi aweze kueleza maendeleo yaliyotokana na matumizi ya chuma. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza mabadiliko ya kimaendeleo katika zama za chuma. | Picha za shughuli mbali mbali za kiuchumi kuonesha matumizi ya zana za chuma. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maendeleo yaliyotokana na matumizi ya chuma? | 3 |
| 2. MIFUMO YA KIUCHUMI NA KIUTAWALA KATIKA ZANZIBAR NA | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza maana ya ujima. | Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya ujima. | 1. Makala kuhusu ujima.<br>2. Makala kuhusu ujima yaliyoandikwa | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maana ya ujima? | 6 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| TANGANYIKA HADI 1880.<br>a) Ujima. | | | kwa Braille. | | |
| | (ii) Kuorodhesha sifa za ujima. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma maandiko yanayohusu sifa za ujima.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kuorodhesha sifa za ujima. | 1. Makala kuhusu ujima.<br><br>2. Makala kuhusu ujima katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuorodhesha sifa za ujima? | |
| | (iii) Kueleza shughuli za kiuchumi wakati wa ujima. | Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza shughuli za kiuchumi wakati wa ujima. | 1. Picha za shughuli za kiuchumi wakati wa ujima.<br>2. Picha mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza shughuli za kiuchumi wakati wa ujima? | |
| | (iv) Kueleza aina ya uongozi katika mfumo wa ujima. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza aina ya uongozi katika mfumo wa ujima. | 1. Picha ya kiongozi wa ukoo akihutubia watu wa ukoo wake.<br>2. Picha mguso ya | Je, mwanafunzi anaweza kueleza aina ya uongozi katika mfumo wa ujima? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza aina ya uongozi katika mfumo wa ujima. | kiongozi wa ukoo.<br>3. Kielelezo cha muundo wa uongozi katika mfumo wa ujima.<br>4. Kielelezo mguso cha muundo wa uongozi katika ujima. | | |
| b) Ukabaila/Umwinyi. | Mwanafunzi aweze:<br>(i)Kueleza maana ya ukabaila/umwinyi. | Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya ukabaila/umwinyi. | Picha ya nokoa akifanya kazi katika shamba la kabaila/ mwinyi. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maana ya ukabaila/ umwinyi? | 5 |
| | (ii) Kuorodhesha sifa za ukabaila/umwinyi. | Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kuorodhesha sifa za ukabaila/ umwinyi. | 1. Kitabu chenye habari kuhusu mfumo wa ukabaila/umwinyi.<br>2. Makala katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuorodhesha sifa za ukabaila/ umwinyi? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iii) Kueleza shughuli za kiuchumi katika mfumo wa ukabaila /umwinyi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu atoe vidokezo vya shughuli za kiuchumi katika mfumo wa ukabaila /umwinyi.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza shughuli za kiuchumi katika mfumo wa ukabaila/umwinyi. | 1. Picha za shughuli za kiuchumi katika mfumo wa ukabaila/umwinyi.<br>2. Picha mguso za shughuli za kiuchumi katika umwinyi/ukabaila. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza shughuli za kiuchumi katika mfumo wa ukabaila/ umwinyi? | |
| | (iv) Kueleza aina ya utawala katika mfumo wa ukabaila/umwinyi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kukusanya taarifa kuhusu aina ya utawala katika mfumo wa ukabaila/umwinyi.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza aina ya utawala katika mfumo | 1. Makala mbali mbali kuhusu mfumo wa ukabaila umwinyi.<br>2. Makala katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza aina ya utawala katika mfumo wa ukabaila/ umwinyi? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | wa ukabaila/umwinyi. | | | |
| 3. UINGIAJI WA WAGENI ZANZIBAR<br>a) Wageni Kutoka Asia Walioingia Zanzibar. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja wageni wa awali walioingia Zanzibar kutoka Asia. | Kwa kutumia mbinu ya masimulizi mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja wageni wa awali walioingia Zanzibar kutoka Asia. | 1. Ramani ya Dunia.<br>2. Ramani mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja wageni wa awali walioingia Zanzibar kutoka Asia? | 5 |
| | (ii) Kueleza namna wageni kutoka Asia walivyokuja Zanzibar. | Kwa kutumia mbinu ya utafiti mdogo mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza namna wageni kutoka Asia walivyokuja Zanzibar. | 1. Ramani ya dunia inayoonesha pepo za msimu.<br>2. Ramani mguso.<br>3. Picha ya jahazi.<br>4. Picha/mchoro mguso.<br>5. Majahazi halisi. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza namna wageni kutoka Asia walivyokuja Zanzibar? | |
| | (iii) Kutaja bidhaa zilizoletwa na wageni kutoka Asia na zile zilizochukuliwa kutoka Zanzibar. | Kwa kutumia mbinu ya ziara ya kimasomo mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha bidhaa mbali mbali zilizoletwa na wageni kutoka Asia na zile zilizochukuliwa kutoka | 1. Picha za bidhaa mbali mbali kutoka Asia na Zanzibar.<br>2. Picha mguso.<br>3. Bidhaa halisi. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja bidhaa zilizoletwa kutoka Asia na zile | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Zanzibar. | | zilizochukuliwa kutoka Zanzibar? | |
| | (iv) Kueleza athari za kuingia kwa wageni kutoka Asia. | Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza athari za kuingia kwa wageni Zanzibar. | 1. Makala yanayohusu biashara kati ya Asia na Zanzibar.<br>2. Makala katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza athari za kuingia kwa wageni kutoka Asia? | |
| b) Biashara ya Watumwa Afrika Mashariki. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza maana ya biashara ya watumwa. | 1. Kwa kutumia mbinu ya filamu inayohusu biashara ya utumwa mwalimu awaongoze wanafunzi kutafakari maana ya biashara ya watumwa.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya biashara ya watumwa. | Filamu ya biashara ya watumwa. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maana ya biashara ya watumwa? | 3 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kueleza sababu zilizopelekea kuibuka kwa biashara ya watumwa. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi mwalimu atoe vidokezo vya sababu za kuibuka kwa biashara ya watumwa.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza sababu zilizopelekea kuibuka kwa biashara ya watumwa. | 1. Makala kuhusu biashara ya watumwa.<br>2. Makala katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza sababu zilizopelekea kuibuka kwa biashara ya watumwa? | |
| c) Wageni kutoka Ulaya Walioingia Zanzibar. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja wageni walioingia Zanzibar kutoka Ulaya. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja wageni walioingia Zanzibar kutoka Ulaya. | 1. Ramani ya dunia.<br>2. Ramani mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja wageni walioingia Zanzibar kutoka Ulaya? | 5 |
| | (ii) Kueleza namna wageni walivyokuja Zanzibar kutoka Ulaya. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza namna wageni walivyokuja Zanzibar kutoka Ulaya. | 1. Ramani ya dunia inayoonesha pepo za msimu.<br>2. Ramani mguso.<br>3. Picha mguso za | Je, mwanafunzi anaweza kueleza namna wageni walivyokuja | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | meli.<br>4. Picha za meli. | Zanzibar kutoka Ulaya? | |
| | (iii) Kutaja bidhaa walizokuja nazo wageni kutoka Ulaya na zilizochukuliwa Zanzibar kupelekwa Ulaya. | Kwa kutumia mbinu ya ziara ya kimasomo mwalimu awaongoze wanafunzi kuainisha bidhaa zilizoletwa na wageni kutoka Ulaya na zilizochukuliwa Zanzibar kupelekwa Ulaya. | 1. Picha za bidhaa mbali mbali Ulaya na Zanzibar.<br>2. Picha/michoro mguso ya bidhaa za Ulaya na Zanzibar.<br>3. Nyumba za makumbusho. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja bidhaa walizokuja nazo wageni kutoka Ulaya na zilizochukuliwa Zanzibar kupelekwa Ulaya? | |
| | (iv) Kueleza sababu za kuja kwa wageni kutoka Ulaya. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza sababu za kuja kwa wageni Zanzibar kutoka Ulaya. | 1. Kitini kinachohusu kuja kwa wageni Zanzibar kutoka Ulaya.<br>2. Kitini katika maandishi ya Braille.<br>3. Kitabu cha kiada.<br>4. Kitabu cha kiada | Je, mwanafunzi anaweza kueleza sababu za kuja kwa wageni Zanzibar kutoka Ulaya? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | katika maandishi ya Braille. | | |
| | (v) Kueleza athari za kuingia kwa wageni kutoka Ulaya. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mbali mbali mwalimu awaongoze wanafunzi kupata maarifa kuhusu kuingia kwa wageni Zanzibar kutoka Ulaya.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza athari za kuingia wageni kutoka Ulaya. | 1. Makala yanayohusu athari za kuingia wageni kutoka Ulaya.<br>2. Makala katika maandishi ya Braille kuhusu athari za kuingia wageni kutoka Ulaya.<br>3. Kitabu cha kiada.<br>4. Kitabu wa kiada katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza athari za kuingia kwa wageni kutoka Ulaya? | |
| 4. UINGIAJI WA WAGENI TANGANYIKA NA ATHARI ZAKE | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja wageni wa awali walioingia Tanganyika kutoka Asia. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja wageni wa awali walioingia Tanganyika kutoka Asia. | 1. Ramani ya dunia.<br>2. Ramani mguso.<br>3. Kitabu cha kiada.<br>4. Kitabu wa kiada katika maandishi | Je, mwanafunzi anaweza kutaja wageni wa awali walioingia Tanganyika | 5 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| a) Wageni kutoka Asia Walioingia Tanganyika. | | | ya Braille. | kutoka Asia? | |
| | (ii) Kueleza namna wageni walivyokuja kutoka Asia. | Kwa kutumia mbinu ya kujisomea makala na vitabu mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza namna wageni walivyokuja kutoka Asia. | 1. Ramani inayoonesha pepo za msimu.<br>2. Picha za jahazi.<br>3. Picha mguso.<br>4. Kitabu cha kiada.<br>5. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza namna wageni walivyokuja kutoka Asia? | |
| | (iii) Kutaja bidhaa zilizotolewa kutoka Asia na zile zilizotoka Tanganyika kupelekwa Asia. | Kwa kutumia mbinu ya ziara ya kimasomo mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha bidhaa zilizoletwa kutoka Asia na zilizopelekwa Asia kutoka Tanganyika. | 1. Kitabu cha kiada.<br>2. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille.<br>3. Nyumba za makumbusho. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja bidhaa zilizoletwa kutoka Asia na zilizopelekwa Asia kutoka Tanganyika? | |
| | (iv) Kueleza athari za kuingia kwa wageni kutoka Asia. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mbali mbali mwalimu awaongoze wanafunzi | 1. Kitabu cha kiada.<br>2. Kitabu cha kiada katika maandishi ya | Je, mwanafunzi anaweza kueleza athari za | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kupata taarifa kuhusu athari za kuingia kwa wageni Tanganyika.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza athari za kuingia kwa wageni kutoka Asia. | Braille. | kuingia kwa wageni kutoka Asia? | |
| b) Wageni Kutoka Ulaya Walioingia Tanganyika. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja mataifa ya Ulaya yaliyoingia Tanganyika. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja mataifa ya Ulaya yaliyoingia Tanganyika. | 1. Ramani ya dunia.<br>2. Ramani mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja mataifa ya Ulaya yaliyoingia Tanganyika? | 4 |
| | (ii) Kubainisha sababu za kuingia kwa wageni kutoka Ulaya. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kupata maarifa kuhusu sababu za kuingia wageni Tanganyika kutoka Ulaya.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya | 1. Makala kuhusu sababu za kuingia kwa wageni kutoka Ulaya kuja Tanganyika.<br>2. Makala katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kubainisha sababu za kuingia kwa wageni kutoka Ulaya? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha sababu za kuingia wageni Tanganyika kutoka Ulaya. | | | |
| | (iii) Kueleza athari za kuingia Tanganyika wageni kutoka Ulaya. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kupata maarifa juu ya athari za kuingia kwa wageni kutoka Ulaya.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza athari za kuingia Tanganyika wageni kutoka Ulaya. | 1. Makala kuhusu athari za wageni kutoka Ulaya.<br>2. Makala katika maandishi ya Braille.<br>3. Kitabu cha kiada.<br>4. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza athari za kuingia Tanganyika wageni kutoka Ulaya? | |
| 5. VITANGULIZI VYA UKOLONI<br>a) Maana ya Vitangulizi vya Ukoloni. | (i) Mwanafunzi aweze kueleza maana ya vitangulizi vya ukoloni. | Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya vitangulizi vya ukoloni. | 1. Kitini kinachohusu vitangulizi vya ukoloni. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maana ya vitangulizi vya ukoloni? | 3 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2. Kitini katika maandishi ya Braille. | | |
| b) Makundi ya Vitangulizi vya Ukoloni. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kubainisha makundi ya vitangulizi vya ukoloni na mifano yake. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha makundi ya vitangulizi vya ukoloni.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha makundi tofauti ya vitangulizi vya ukoloni. | 1. Makala yenye maandiko yanayohusu vitangulizi vya ukoloni.<br>2. Makala katika maandishi ya Braille.<br>3. Picha za vitangulizi vya ukoloni.<br>4. Picha mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kubainisha makundi tofauti ya vitangulizi vya ukoloni na mifano yake? | 4 |
| | (ii) Kueleza madhumuni ya kila kikundi na athari zake. | 1. Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza madhumuni ya kila kikundi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya | 1. Vitini na vitabu kuhusu madhumuni ya makundi ya vitangulizi vya ukoloni. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza madhumuni ya kila kikundi na athari zake? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | changanya kete mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza athari za kila kikundi. | 2. Vitini na vitabu katika maandishi ya Braille. | | |
| 6. KUGOMBANIWA NA KUGAWANYWA KWA AFRIKA<br>a) Mabeberu Kugombania Afrika. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza maana ya ubeberu. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya ubeberu. | 1. Kitabu cha kiada.<br>2. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maana ya ubeberu? | 4 |
| | (ii) Kutaja mataifa ya Ulaya yaliyogombania Afrika. | Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja mataifa ya Ulaya yaliyogombania Afrika. | 1. Ramani ya nchi za Ulaya.<br>2. Ramani mguso.<br>3. Makala mbali mbali zinazohusu mataifa ya Ulaya yaliyogombania Afrika. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja mataifa ya Ulaya yaliyogombania Afrika? | |
| | (iii) Kueleza sehemu za Afrika zilizogombaniwa zaidi na sababu zake. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kusoma ramani mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza sehemu za Afrika zilizogombaniwa zaidi na sababu zake. | 1. Ramani ya Afrika inayoonesha sehemu zilizogombaniwa na mabeberu.<br>2. Ramani mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza sehemu za Afrika zilizogombaniwa zaidi na sababu | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kuonesha na kuorodhesha sehemu za Afrika zilizogombaniwa zaidi na sababu zake. | 3. Makala na vitabu kuhusu sehemu za Afrika zilizogombaniwa zaidi.<br>4. Maandiko katika maandishi ya Braille. | zake? | |
| | (iv) Kuchora ramani ya Afrika kuonesha maeneo yaliyogombaniwa zaidi. | Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko yenye ramani ya Afrika mwalimu awaongoze wanafunzi kuchora ramani ya Afrika kuonesha maeneo yaliyogombaniwa zaidi. | 1. Ramani ya Afrika kuonesha maeneo yaliyogombaniwa zaidi.<br>2. Ramani mguso.<br>3. Vifaa vya kuchorea ramani.<br>4. Mashine ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuchora ramani ya Afrika kuonesha maeneo yaliyogombaniwa zaidi? | |
| b) Mabeberu Kugawana Afrika. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kuelezea madhumuni ya mkutano wa Berlin wa 1884 – 1885. | Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza madhumuni ya mkutano wa Berlin wa 1884 – | 1. Makala kuhusu Mkutano wa Berlin wa 1884 – 1885. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza madhumuni ya | 3 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 1885. | 2. Makala katika maandishi ya Braille.<br>3. Ramani ya Ujerumani inayoonesha mji wa Berlin.<br>4. Picha ya Chancellor Bismark.<br>5. Picha mguso. | Mkutano wa Berlin wa 1884 – 1885? | |
| | (ii) Kujadili sababu zilizopelekea mataifa ya Ulaya kugawana bara la Afrika. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kazi maalum mwalimu awaongoze wanafunzi kukusanya taarifa kuhusu sababu za mataifa ya Ulaya kugawana Bara la Afrika.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya pamoja mwalimu awaongoze wanafunzi kujadili sababu zilizopelekea mataifa ya Ulaya kugawana Bara la Afrika. | 1. Nakala za maswali ya kujadili.<br>2. Maswali katika maandishi ya Braille.<br>3. Makala kuhusu sababu zilizopelekea mataifa ya Ulaya kugawana Afrika.<br>4. Makala katika | Je, mwanafunzi anaweza kujadili sababu zilizopelekea mataifa ya Ulaya kugawana bara la Afrika? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | maandishi ya Braille. | | |
| 7. UVAMIZI WA KIKOLONI ZANZIBAR NA TANGANYIKA<br>a) Uvamizi Zanzibar na Tanganyika. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja mataifa yaliyovamia na kutawala Zanzibar na Tanganyika. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja mataifa yaliyovamia na kutawala Zanzibar na Tanganyika. | 1. Kitabu cha kiada.<br>2. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja mataifa yaliyovamia na kutawala Zanzibar na Tanganyika? | 4 |
| | (ii) Kueleza sababu za uvamizi wa kikoloni Zanzibar naTanganyika. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kupata maarifa kuhusu sababu za uvamizi wa kikoloni Zanzibar na Tanganyika.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya matembezi ya ukumbini mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza sababu za uvamizi wa kikoloni Zanzibar na | 1. Makala kuhusu sababu za uvamizi wa kikoloni Zanzibar na Tanganyika.<br>2. Makala katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza sababu za uvamizi wa kikoloni Zanzibar na Tanganyika? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Tanganyika. | | | |
| | (iii) Kueleza mbinu zilizotumika kufanya uvamizi Zanzibar naTanganyika. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko katika vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kujadiliana na kuorodhesha mbinu walizotumia wavamizi kuvamia Zanzibar na Tanganyika.<br><br>2. Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza mbinu zilizotumika kufanya uvamizi Zanzibar na Tanganyika. | 1. Makala kuhusu mbinu zilizotumika kufanya uvamizi Zanzibar na Tanganyika.<br>2. Makala ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza mbinu zilizotumika kufanya uvamizi Zanzibar na Tanganyika? | |
| b) Mikataba ya Kuigawa Afrika Mashariki. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kuorodhesha mikataba ya kuigawa Afrika Mashariki. | Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kuorodhesha mikataba ya kuigawa Afrika Mashariki. | 1. Ramani za Afrika Mashariki baada ya mkataba wa 1884 na baada ya mkataba wa 1890.<br>2. Ramani mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kuorodhesha mikataba ya kuigawa Afrika Mashariki? | 4 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | 3. Makala kuhusu mikataba ya kuigawa Afrika Mashariki.<br>4. Makala katika maandishi ya Braille. | | |
| | (ii) Kueleza vipengele vya kila mkataba. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kusoma maandiko mwalimu awaongoze wanafunzi kupata maarifa kuhusu vipengele vya mikataba ya Wajerumani na Waingereza ya mwaka 1886 na 1890.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya matembezi ya ukumbini mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza vipengele vya mikataba ya Wajerumani na Waingereza. | 1. Nakala za mikataba ya kikoloni.<br>2. Mikataba katika maandishi ya Braille.<br>3. Ramani ya Afrika Mashariki baada ya Mkataba wa 1884 na baada ya Mkataba wa 1890.<br>4. Ramani mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza vipengele vya kila mkataba? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
